# Upendano wa Ndugu

(Brotherly Kindness)
*1Yoh 2:9-10*

*Yeye asemaye kwamba yumo nuruni, naye amchukia ndugu yake, yumo gizani hata sasa.Yeye ampendaye ndugu yake, akaa katika nuru wala ndani yake hamna kikwazo.*

*S*ikiliza kile Nabii wa Mungu anasema juu ya hilo**:**

Kama unahitaji kuwa baraka, na kupata baraka, wakati mtu amekutendea vibaya, na amekutendea vibaya hasa, ye…….Namaanisha amekutendea vibaya, nawe unajua amekutendea vibaya, amekutenda maovu usilitaje hilo umchukue yeye kwenye maombi mbele za Mungu.Na usilichukuwe tu katika njia ya kichoyo na kusema, vema ninapaswa kulifanya hili.

Lakini simama bega kwa bega, na usimame katika uwepo wa Mungu Baba yetu, katika njia, maombi yalipaswa yafanywe katika uwepo wa Mungu, sema,'' Baba hapa yuko ndugu yangu, na yeye tu; amestahili adhabu kwa sababu amenitendea uovu..Na sioni kwa nini alifanya hivyo.

Kisha umwache Mungu aende kukuzungumzia,na labda utaona, pengine kile mtu yule amepitia shetani amempotosha mahali fulani na kumsababishia atende hivyo .Ingawa amekosea kabisa, kabla hujaondoka kwenye kiti cha Mungu utajisikia huzuni juu ya mtu huyo. Utasikitika pamoja na ndugu huyu.Na utakaporejea tena chini mahali hapa duniani tena, utamuendea ndugu huyo na kupeana naye mikono, kwa sababu unajua kile amepitia.

Huwezi kusimama na binadamu katika uwepo wa Mungu na kumhukumu mtu yoyote. Siamini, hapana, bwana, hata kama yeye ni mwenye dhambi mkuu sana.

Na vipi kuhusu ndugu ambaye amefanya makosa? Ingawaje nasema yuko makosani wakati mwingine ameshitakiwa kosa wakati yeye hayuko makosani.Lakini ikiwa amekosea, vema, kama tutamchukuwa hadi mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, tukisimama pale bega kwa bega pamoja na ndugu yetu, tukijua yeye ni apatikanaye na mauti na labda kikomo chake kiko juu ya mtazamo wetu dhidi yake, tunaporejea tena kutoka mbele ya kiti cha enzi cha Mungu.Tunatambua kila mmoja wetu ana hatia na tunahitaji msaada wa mmoja kwa mwingine na njia bora ya kufanya ni kuomba.

Sawa.Tukija katika ukamilifu sasa…….sawa hisi sita, acha tuongeze.Biblia inasema hapa, tieni (ongezeni) upendano wa ndugu……Upendano wa ndugu (2Petro 1:3-11) sasa hilo ni jema, papa hapa, ya sita……..saba sawa, tieni (ongezeni) upendano wa ndugu sawa. Tutakapofikia huo upendano wa ndugu, jiweke mwenyewe katika mahali pake juu ya jambo hilo(Luka 6:31).Sasa, unasema.`` ndugu yangu amenikosa, Petro akamwambia, je nimsamehe? Akasema hata mara saba kwa siku? Mathayo 18:21-22**.**

Huwezi kuwarejesha tena kwa Kristo, na ikiwa huwezi kufanya hivyo, Basi umwambie mtu mwingine, au waache waende pamoja nawe. Lifanye katika njia, maandiko yamesema.(Mathayo18;15-17).

Ikiwa mtu fulani akisema,'' Dada fulani na fulani, au ndugu fulani la fulani, usiamini hata Neno moja ya hilo. Liache tu liende, kwa sababu, kumbuka ni ibilisi akijaribu kuwararua vipande vipande.Sasa mtazamieni tu (kuja), sababu atafanya hivyo.Sasa muacheni mtu aliye mwema wa nyumba, Imani isimame tu pale, na usipokee hata kitu kimoja.Watu hawa wamewekwa katika ulimwengu wa Roho pamoja nawe, mkishiriki pamoja kuzunguka baraka za Mungu, mkichukua ushirika mezani na Roho Mtakatifu ameshuhudia kuwa wao ni watoto wa Mungu. Hivyo uwe tu mtamu mwenye moyo wa huruma, mwenye kusamehe, mwenye upendo.Na kama ikiwa mtu mwingine atanena maovu dhidi yako, wewe nena vema dhidi yao kisha tazama jinsi ilivyo vyema, yatakavyo kurejea wakati huo.Hiyo ni kweli.Siku zote rudisha mema kwa maovu, Upendo kwa chuki (Mathayo 5:43-48).

Sasa uwe na uhakika kufanya hivyo, ahidi hilo kwamba Mungu kwa Neema yako, hivyo ndivyo nitakavyo fanya. Haijalishi wakati awaye yote anena maovu; rejesha mema usiwazie uovu kamwe.Kama unawazia maovu, na ukilisema kwa unafiki tu, utakuwa uko makosani.Wewe endelea tu kujiweka wakfu mbele za Mungu mpaka unapojisikia vema juu ya mtu huyo.Hiyo ndio njia ya kulitenda hilo . Kisha wema wa baraka za Mungu utafunika nafsi yako. Na hiyo ndio njia ya kuishi mshindi, kisha hakuna kitu cha kukudhuru ilimradi uko katika upendo (1Yohana 4:16).

Unaona, kama kuna lugha, zitakoma. Na kama una hekima, zitatoweka. Unabii utashindwa. Lakini wakati unapopata Upendo, utadumu milele (1Kor 13:1-10) unaona?

Na usiwapende tu wale wanaokupenda, lakini uwapende wale ambao hawakupendi. Kwa kuwa ni rahisi kumpenda mtu yeyote ambaye anakupenda, lakini kujaribu kumpenda mtu ambaye hakupendi. Hapo unaweza kujijaribu kama wewe ni Mkristo au siyo. Mtu fulani ambaye hakupendi wewe na bado moyoni mwako unampenda na kama hufanyi hivyo endelea kumshikilia Mungu, liko hapo, sababu najua hili kuwa ni kweli. Amina. Najua hiyo ni kweli.

Kuna wakati mwingi ambapo mhudumu atafanya kosa, na akija katika mtaa huo wa majirani, ndugu mpendwa anaye jaribu kufanya yaliyo kweli na kuwaongoza watu kwa haki, kila kitu ambacho shetani anaweza kumuelekeza kwa asiye amini ama anayedai kuwa Mkristo katika mtaa huo, kumtupia mtu huyo, yeye atafanya hivyo. Unajua, njia halisi ya Ukristo ni kuficha kila uwezacho kutoka kwa ndugu, usiseme mambo yake mabaya: Sema tu mambo yake mazuri. Sema tu yale unayojua kumhusu ambayo ni mema, Chochote kibaya kiache, masikini mtu huyo ana mengi ya hutosha dhidi yake, haidhuru usijaribu kuchukuwa mti ukamsukumizia mtu huyo upande wa ndani sana wa shimo.Mtazamo wa Kikristo ni kumwinua juu na kumtoa kwenye shimo unaona? Usijaribu kama kumpiga kikumbo yuko chini tayari, jaribu kumsaidia aamke bali wengi wenu siku hizi, watu wengi sana leo.Naweza kusema wanajaribu kufanya hivyo. Kama wangelipata jambo fulani ambalo lilikuwa baya sana wangelilisema.

Alisema saba mara sabini!! Unaona, Upendano wa ndugu sasa, unaona kama ndugu yako yuko nje ya utaratibu, usikose kuwa na subira naye, unaona? Hapana. unaona? Kuwa mkarimu kwake na umuendee kwa vyovyote.

Mtu fulani alisema si muda mrefu uliopita,alisema,’’ unawezaje kuamini mambo hayo katika njia ufanyayo na bado uende Asembies of God, na wa umoja na wengineo wote? Vema, unaona? Upendano wa ndugu, unakufanya utumainie kwamba siku moja, Unaona? Subira naye, kiasi, vumilia pamoja naye, maarifa ya kuelewa kile anachoamini nakumbuka kiko moyoni mwake hivyo ndivyo ilivyo nguvu ndani yako kuiacha itoke na ukarimu na upole kwake; ukiwa na imani kwamba siku moja Mungu atamleta yeye ndani, unaona? Upendano wa Ndugu,’’‘’Huwezi kuniacha nje, maana ninawapenda mnaona, hamwezi kufanya hivyo kamwe’’ nikasema kuna wengi sana wa ndugu ze-zenu huko nje wanaonipenda mimi na wananiamini’’ nikasema………Wao watakuja, hata hivyo’ nikasema,’’ watakuja.wala huwezi kuniacha nje. Kama mkiniacha nje.Mimi nitawavuta ndani tena‘‘ Nikasema,’’ Mnapochora mviringo mmoja, Mungu, kwa neema yake,atanijalia kuchora mwingine na kuwa ingiza moja kwa moja ndani tena**.**

Nimejaribu kila mara kadri niwezavyo katika kuto kukubaliana na watu katika mambo ya kidini;lakini kama singeweza kumsalimia kwa mkono baadaye, haijalishi lingelikuwa jambo kali vipi, na kumsalimia kwa mkono kwa kusema, hii ni katika nuru ya kuelewana vema kati yetu, ‘‘ nami bado nampenda mtu huyo si kusema tu kwa kinywa changu, lakini kwa moyo wangu, ndipo si-paswi kwenda nje na kujaribu kuzungumza na watu.Kwa sababu, mwaona,lazima tutende hivyo, lazima tumpende mtu huyo.Mwaona? na kuendelea kati ya watu wa kila tabaka na madhehebu na makabila mbali mbali, na dini na kadhalika, na kujaribu kuiweka Biblia chini, na kusema‘‘ hebu na tujadiliane si kwa kanuni zako za imani wala kwa vitabu vyenu vya elimu ya maadili, kwa Biblia!! Na ndipo……Labda wakati mwingine mtu hunena kwa ukali sana; lakini ikiwa nina wazo moja kuwa sikumpenda mtu huyo, basi- basi unajua jambo moja, Roho wa Kristo ameondoka kwangu. Ikiwa naweza kujisikia simpendi mtu huyo kuna kasoro kwangu.

Kwa sababu Roho wa Kristo, wakati wao…….katika kumsulubisha Yeye, na watu wake mwenyewe wakimpigilia misumari,na…..viumbe wale aliowaumba wakimpigilia misumari, wale Yeye aliowaumba wakirudisha misumari ndani ya mwili wake wa binadamu.Walakini, akiwa na moyo uliojaa Upendo akilia, Baba uwasamehe, hawajui watendalo, mwaona? (Yoh 19:30).

Sasa ,usisikilize chochote kimojawapo kiovu ibilisi ambacho atapata kusema mnaona? Ikiwa Ibilisi atakuonyesha mambo,au akwambie kitu kiovu juu ya mmoja wa washirika wa ule mwili wa Kristo usiamini hilo.Kwa kuwa mara tu utakapo uamini, unaharibu(ushuhuda) ujuzi wako.

Na ikiwa utamwona mmoja wa washirika wa mwili wa Kristo akifanya uovu, usimwambie mtu yoyote mwingine; lakini mwendee mshirika huyo, na kwa Upendo uone kama……..

Sasa kwa mfano, kama-kama mmoja wenu ndugu angelifanya kosa na kufanya jambo baya-ambalo unaweza kufanya; mimi pia, kila mmoja wenu.Bali tunapoendelea, hebu na tukumbuke sisi ni ndugu. Na iwapo

tuna vita vyovyote, hebu tupigane sisi kwa sisi.Vileteni pamoja mbele ya ndugu zetu mkavisuluhishe.

Sasa katika jamaa ya Branhamu walizoea hilo, kama mmoja wao watoto alifanya jambo fulani wangemwambia Bill juu yake,maana mimi ndiye niliyekuwa mkubwa. Nami ikinibidi kusimama pale na kuona ni nani aliyekuwa sahihi na nani mwenye hatia. Vema uamuzi wangu ulikuwa ya kwamba kama bado hawakuamini hilo wangerudi nyuma yangu na kupiga-na kisiri.Bali hata hivyo wao walikuwa wangali ndugu mnaona? Wao wangepigana nyuma ya nyumba wao kwa wao na kupigana mbele ya nyumba wao kwa wao.Kwa hiyo ndivyo ilikuwa, na tungali ndugu.

Vema, hivyo—ndivyo inatupasa kufanya hayo unaona? Na kama una neno dhidi ya mtu fulani, ndugu yako usimwambie mtu mwingine.juu ya hilo kama siyo sahihi,nenda ukamuone na umueleze Ndipo iwapo atabishana nawe, basi mchukuwe mtu mwingine mwende naye. Kisha ifanye jinsi Biblia ilivyo sema.

Tunapoona ishara kuu za mwisho, na wakati-unakaribia, ukituonya wakati umekaribia’’

Jamani chukulieni hili kwa uchaji; inatupasa kupendana sisi kwa sisi .Lo, jamani! inapasa kupendana sana! Msinene maovu ninyi kwa ninyi. Mtu akitenda kosa muombeeni upesi sana!.Tuko pamoja katika hili, pamoja na Mungu, sisi ni kaka na dada ishini kitakatifu ishini mkiwa wazuri, wakarimu na wanyenyekevu.

Hebu uovu wowote usiingie mawazoni mwenu, katika fikra zenu.Uondoeni tu.(Wafilipi 4:8) ukipiga hodi mlangoni uondoeni. Onyesheni ishara yenu, endeleeni tu kutembea,’’ niko chini ya damu;;

Na yawapasa kupendana (Yohana 13: 4-35) waamini wanapaswa kujitenga na ulimwengu.Usiichukuwe sasa kwa urahisi, ninyi watu mnaosikiliza hili, kwenye kanda, enyi wanawake ,enyi wanaume sikilizeni kwa dakika moja kama umewahi kuniamini amini sasa .Ni wakati wa kukomesha kuzozana mmoja kwa mwingine, aminini ujumbe wa Biblia. Muamini Yesu Kristo kisha pendaneni, stahianeni, na heshimianeni. Enyi wanaume waheshimuni wake zenu. Heshimuni nyumba zenu.kusanya jamaa, si mtu mmoja tu, ni jamaa nzima,pia, ilipaswa kuleta kila kitu kuingizwa ndani. Inatupasa kupendana sisi kwa sisi. Nao waamini inawapasa kujitenga na Ulimwengu.

<u>Nukuu</u>

Agizo kuu (58-03-01B)Aya 12-E13 (E.BOOK)
Kimo cha mtu mkamilifu uk,45’’Shalom-AYA 35-41
Hisi kuu –Aya 35-41
Kuchukuwa upande wa Yesu-aya 130-133
Ishara (63-09-01M)uk.34-4(Aya 242-250)

---

*jiwe la kiroho la kujengea na 127 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*